# Wavuvi Tanga hatarini corona

Tanga: Wavuvi na wauzaji wa samaki jijini hapa wapo katika hatari ya kukumbwa na maambukizi ya corona kutokana na baadhi ya wateja wao kugoma kuvaa barakoa wala kunawa mikopo.

Kutokana na hali hiyo, wameiomba Serikali kuingilia kati sakata hilo kwa kuwaelimisha wateja wao ili kuwanusuru na maambukizi.

Said Mbezi anayaeuzia samaki katika soko la Deap Sea aliisema tangu tahadhari ya kujikinga itolewe wanajitahidi kuwaeleza wateja wao bila mafanikio.

"Kama unavyoona samaki ni wachache sana hivyo wateja wanagombea ukimwambia anawe mikono anakwamba hawezi kwani eneo lenyewe ni nichafu," alisema Mbezi.

**(Rais Said)**

ku

ha
kw
ku
w
hi
w
aj
Ja

ut
w
zo
hi
w
ki

sp
al
fe
ta

ya
no

Ra
ga
se
da
no

Scanned by CamScanner

# Kikundi cha vijana chapewa vifaranga vya kuku 540

Na Mwandishi Maalumu

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imewapa vifaranga vya kuku 540 kikundi cha vijana wajasiriamali ili kuhamasisha ufugaji utakaosaidia kuziba pengo la uhaba wa nyama ifikapo mwaka 2022 pamoja na kukuza sekta ya kuku nchini.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Mazao ya Mifugo na Usalama wa Chakula na Lishe wa wizara hiyo, Gabriel Bura alikabidhi vifaranga hivyo mwishoni mwa wiki kwa wawakilishi wa kikundi cha vijana watatu wajasiriamali jijini Dar es Salaam.

Bura alisema hatua hiyo inatokana na mkutano uliofanyika kati ya Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Profesa Elisante Ole Gabriel na wadau wa tasnia ya kuku kilichoketi Machi 7 mwaka huu katika ofisi ndogo za wizara hiyo zilizopo jijini Dar es Salaaam.

Kwa mujibu wa Bura, Profesa Gabriel alimsikiliza mdau mmoja mmoja, lakini alishawishika zaidi na uwepo wa vijana wenye umri wa chini ya miaka 35 walioonesha nia ya kuwekeza katika tasnia ya ufugaji wa kuku.

Mbali na hilo, Bura alisema hatua hiyo pia ni sehemu ya kutekeleza mpango mkakati wa wizara hiyo ya kuhamasisha ufugaji wa kuku kwa vikundi vya vijana na akinamama.

Aidha alisema vijana hao wameonesha uthubutu na wameonekana kupenda tasnia hiyo ili kukabiliana na hali halisi ya soko la ajira, akisema baadhi yao wamesomea fani ya sheria na wengine habari na mawasiliano.

Alifafanua kuwa mpango wa kuhamasisha ufugaji wa kuku, katibu mkuu aliamua kuanza na vijana watatu ambao watakuwa chachu kwa wenzao kujifunza.

Alisema serikali imeamua kuwapatia vifaranga vya kuku 540, pamoja na vyakula vya mwezi mmoja, chanjo, vilishio na vinywesheo ambapo msaada huo umegharimu Sh milioni 6.1

Kwa mujibu wa Bura, mpango kabambe wa miaka 15 wa kuendeleza sekta ya mifugo umeonesha kuwa kutakuwa na upungufu wa nyama unaokaridiwa tani ya zaidi ya 100,000 ifikapo mwaka 2022 kadri kipato cha wananchi kinavyoongezeka.

"Tumeona huu upungufu wa nyama tunaweza kuufidia katika ufugaji wa kuu ambapo ndani ya miezi miwili au mitatu nyama inapatikana, ndiyo maana serikali imeamua kuongeza nguvu na kuchukua hatua za uhamasishaji zaidi kwa vikundi vya vijana," alisema.

Alisema wameanzia Mkoa wa Dar es Salaam, kisha watakwenda wilayani Mkuranga, mikoa ya Mbeya, Morogoro na Dodoma akisema ni mchakato endelevu wa kutoa vifaranga kwa vikundi vya vijana wajasiriamali.

Sarah Urio ambaye ni msambazaji wa viranga hivyo kutoka kampuni ya AKM Glitters, aliwashukuru vijana kwa kuonesha utayari na uthubutu wa kufuga kuku, akisema licha ya kupewa vifaranga hivyo, lakini uongozi wa kampuni hiyo utakuwa bega kwa bega kwa kuwapa elimu ya namna ya kuendeleza mchakato huo.

Leah Tesha ambaye anaunda kikundi hicho aliishukuru serikali kwa kuwapatia vifaranga hivyo akisema wametimiza ahadi yao na kwamba kuku hao itakuwa kama ajira kwao kwa sababu suala hilo limekuwa ni changamoto kwa vijana wengi.

Alisema wameamua kuthubutu kwa kuandaa mpango mkakati waliouwasilisha katika ofisi ya katibu mkuu wa wizara namna walivyojipanga katika mchakato wa ufugaji wa kuku.

Scanned by CamScanner

# Vijana wahamasishwa ufugaji kuku kujikwamua

**Na MWANDISHI WETU -DAR ES SALAAM**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imewapa vifaranga vya kuku 540 kikundi cha vijana wajasiriamali ili kuhamasisha ufugaji utakaosaidia kuziba pengo la uhaba wa nyama ifikapo mwaka 2022 pamoja na kukuza sekta ya kuku nchini.

Makabidhiano hayo yalifanywa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Mazao ya Mifugo na Usalama wa Chakula na Lishe wa wizara hiyo, Gabriel Bura kwa wawakilishi wa kikundi cha vijana watatu wajasiriamali hafla ilifanyika Mbweni.

Bura alisema kuwa hatua hiyo inatokana na mkutano uliofanyika kati ya Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) Profesa Elisante Ole Gabriel na wadau wa tasnia ya kuku kilichoketi Machi 7, mwaka huu katika ofisi ndogo za wizara hiyo zilizopo jijini Dar es Salaaam

Kwa mujibu wa Bura, Prof. Gabriel alimsikiliza mdau mmoja mmoja, lakini alishawishika zaidi na uwepo wa vijana wenye umri wa chini ya miaka 35 walioonyesha nia ya dhati ya kuwekeza katika tasnia ya ufugaji wa kuku.

Aidha alisema vijana hao wameonyesha uthubutu na wameonekana kupenda tasnia hiyo ili kukabiliana na hali halisi ya soko la ajira akisema baadhi yao wamesomea fani ya sheria na habari na mawasiliano.

"Serikali imeamua kuwapatia vifaranga vya kuku 540, pamoja na vyakula vya mwezi mmoja, chanjo, vilishio na vinywesheo ambapo msaada huo umegharimu Shilingi milioni 6.1

"Mpango kabambe wa miaka 15 wa kuendeleza sekta ya mifugo umeonyesha kuwa kutakuwa na upungufu wa nyama unaokaridiwa tani ya zaidi ya 100,000 ifikapo mwaka 2022 kadri kipato cha wananchi kinavyoongezeka," alisema

Alisema wameanzia Mkoa wa Dar es Salaam, kisha watakwenda wilayani Mkuranga , mikoa ya Mbeya , Morogoro na Dodoma akisema ni mchakato endelevu wa kutoa vifaranga kwa vikundi vya vijana wajasiriamali.

– PICHA: MPIGAPICHA WETU

Scanned by CamScanner

**Lengo>>**Kukabiliana na uhaba wa nyama ifikapo mwaka 2022

# Wizara yatoa vifaranga vya kuku 540 kwa kikundi cha vijana

**Na MWANDISHI WETU**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imetoa vifaranga vya kuku 540 kwa kikundi cha vijana wajasiriamali ili kuhamasisha ufugaji utakaosaidia kuziba pengo la uhaba wa nyama ifikapo mwaka 2022 na kukuza sekta ya kuku nchini.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Mazao ya Mifugo na Usalama wa Chakula na Lishe wa wizara hiyo, Gabriel Bura, alikabidhi vifaranga hivyo mwishoni mwa wiki iliyopita kwa wawakilishi wa kikundi cha vijana watatu wajasiriamali katika hafla iliyofanyika Mbweni jijini Dar es Salaam.

Bura alisema hatua hiyo inatokana na mkutano uliofanyika kati ya Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) Profesa Elisante Ole Gabriel na wadau wa tasnia ya kuku kilichoketi Machi 7, mwaka huu katika ofisi ndogo za wizara hiyo zilizopo jijini Dar es Salaaam

Kwa mujibu wa Bura, Profesa Gabriel alimsikiliza mdau mmoja mmoja, lakini alishawishika zaidi na uwepo wa vijana wenye umri wa chini ya miaka 35 walioonyesha nia ya dhati ya kuwekeza katika tasnia ya ufugaji wa kuku.

Mbali na hilo, Bura alisema hatua hiyo pia ni sehemu ya kutekeleza mpango mkakati wa wizara hiyo ya kuhamasisha ufugaji wa kuku kwa vikundi vya vijana na kina mama.

Aidha, alisema vijana hao wameonyesha uthubutu na wameonekana kupenda tasnia hiyo ili kukabiliana na hali halisi ya soko la ajira akisema baadhi yao wamesomea fani ya sheria na habari na mawasiliano.

Alifafanua kuwa mpango wa kuwahamasisha ufugaji wa kuku katibu mkuu huyo, aliamua kuanza na vijana watatu ambao watakuwa chachu kwa wenzao kujifunza.

Alisema serikali imeamua kuwapatia vifaranga vya kuku 540, pamoja na vyakula vya mwezi mmoja, chanjo, vilishio na vinywesheo ambapo msaada huo umegharimu sh milioni 6.1

Kwa mujibu wa Bura, mpango kabambe wa miaka 15 wa kuendeleza sekta ya mifugo umeonyesha kuwa kutakuwa na upungufu wa nyama unaokaridiwa tani ya zaidi ya 100,000 ifikapo mwaka 2022 kadri kipato cha wananchi kinavyoongezeka.

"Tumeona huu upungufu wa nyama tunaweza kuufidia katika ufugaji wa kuku ambapo ndani ya miezi 2 au 3 nyama inapatikana, ndiyo maana serikali imeamua kuongeza nguvu na kuchukua hatua za uhamasishaji zaidi kwa vikundi vya vijana," alisema.

Aliongeza kuwa hatua nzuri ya kuigwa kwa vijana hao kujihusisha na ufugaji ili kuondokana ile dhana ya kuwa mchakato huo unafanywa na wazee na watu waliostaafu.

Alisema wameanzia Mkoa wa Dar es Salaam, kisha watakwenda wilayani Mkuranga, mikoa ya Mbeya, Morogoro na Dodoma na kwamba ni mchakato endelevu wa kutoa vifaranga kwa vikundi vya vijana wajasiriamali.

Sarah Urio ambaye ni msambazaji wa viranga hivyo kutoka kampuni ya AKM Glitters, aliwashukuru vijana kwa kuonyesha utayari na uthubutu wa kufuga kuku na kusema kuwa licha ya kupewa vifaranga hivyo, lakini uongozi wa kampuni hiyo utakuwa bega kwa bega kwa kuwapa elimu ya namna ya kuendeleza mchakato huo.

"Tukishawapa vifaranga na mahitaji husika hatutawaacha bali tutaendelea kutoa ushirikiano katika mchakato huu. Tutawasimamia mwanzo hadi mwisho ili wafuge kwa ufanisi," alisema

Leah Tesha ambaye anaunda kikundi hicho alishukuru serikali kwa kuwapatia vifaranga hivyo kwa kuwa wametimiza ahadi yao na kwamba kuku hao itakuwa kama ajira kwao kwa sababu suala hilo limekuwa changamoto hivi sasa.

Alisema wameamua kuthubutu kwa kuandaa mpango mkakati waliouwasilisha katika ofisi ya katibu mkuu wa wizara namna walivyojipanga katika mchakato wa ufugaji wa kuku.

"Sisi tumeonyesha njia ni fursa kwa vijana wengine wanaotembea na bahasha mkononi wajitokeze kufuga kuku. Sisi ni mfano vijana wenzetu wanaweza kuga na kuachana na ile dhana wote lazima tupate kazi," alisema.

WAJASIRIAMALI

Scanned by CamScanner

PICHA: MPIGAPICHA WETU





ji

s

**Mjasiriamali, Leah Tesha, akipokea vifaranga vya kuku kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Mazao ya Mifugo na Usalama wa Chakula na Lishe wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Gabriel Bura, kuhamasisha ufuagji wa kuku, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.**

PICHA: MPIGAPICHA WETU

Scanned by CamScanner